

MTIHANI WA DARASA LA NNE MUHULA WA KWANZA 2019

KISWAHILI

SOMA MAAGIZO HAYA KWA MAKINI

1. Hakikisha umeandika

(i) Jina lako

(ii) Jina la shule yako

Muda: Saa 1 Dak. 40

Soma vifungu vifuatavyo, vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila pengo umepewa majibu manne.

Chagua jawabu lifaalo zaidi.

Siku 1 mimi na kaka yangu 2 kumtembelea babu. Tulimkuta nyumbani tukamsamilia 3 babu? akatujibu "Marahaba wajukuu. Baada 4 salamu hizo, babu alitukaribisha shambani kupanda mimea. Babu alituambia kuwa mimea hutupa vyakula 5. Mimea kama mipera hutupatia 6. Baada ya kazi za shambani, tulienda 7 kupata chakula.

Babu alituletea maziwa ya 8 na mihogo, Tulikuwa haraka kwa sababu tulikuwa tukihisi 9 sana. Tulishiba sana na tukamwambia babu 10. Babu alifurahi sana kwa kutembelewa na 11 wake. Tuliamua kurudi nyumbani kwa sababu usiku ulikuwa 12. Babu yetu ni mzee sana ambaye 13 miaka 14 hapa duniani. Tuwaheshimu wazee 15.

- | | | | |
|-----------------|----------------|--------------|----------------|
| 1. A. moja | B. kimoja | C. wamoja | D. mmoja |
| 2. A. nilienda | B. tuliendanga | C. tulienda | D. nimeenda |
| 3. A. habari | B. hujambo | C. sijambo | D. shikamoo |
| 4. A. la | B. za | C. ya | D. wa |
| 5. A. mingi | B. vingi | C. nyingi | D. wengi |
| 6. A. mandazi | B. mayai | C. macembe | D. mapera |
| 7. A. nyumbani | B. msalani | C. maktabani | D. hospitalini |
| 8. A. kuku | B. ng'ombe | C. simba | D. farasi |
| 9. A. jaa | B. kelele | C. njaa | D. nja |
| 10. A. asante | B. pole | C. samahani | D. hodi |
| 11. A. wajukuu | B. wajomba | C. wanafunzi | D. wagonjwa |
| 12. A. anaingia | B. unaingia | C. inaingia | D. zimeingia |
| 13. A. nimeishi | B. tumeishi | C. sijaishi | D. ameishi |
| 14. A. mingi | B. nyingi | C. wengi | D. vingi |
| 15. A. wetu | B. yetu | C. letu | D. zetu |

Kuanzia swali la 16 - 30, chagua jibu sahihi

16. Jibu la alamsiki ni
A. asante B. sajambo
C. vyema D. binuru
17. Tumia **kashiria** sahihi
Mwambie **mwanafunzi** _____ aje hapa.
A. hicho B. hilo
C. lile D. huyo

18. Andika kwa wingi

- Mwalimu huyu anasoma.
A. Walimu wao wanasoma.
B. Walimu wale wanasoma.
C. Walimu hawa wanasoma.
D. Walimu huyo hasomi.

19. **Kanusha**
Tutakunywa maziwa.
A. Hatutakunywa maziwa
B. Hatunywi maziwa
C. Hatukunywi maziwa
D. Hamtakunywa maziwa:

20. Kifaa cha kukunia nazi ni
A. mchi
B. kinu
C. mbuzi
D. uteo


21. Jina "kipepeo liko katika ngeli ya
A. ki-vi
B. i-zi
C. li-ya
D. a-wa

22. Andika kwa maneno 594
A. Mia tano tisini na nne
B. Mia tano sitini na nane
C. Mia tano themanini na nne
D. Mia tano tisini na nane.

23. Tegua kitendawili
Nanywa supu nyanta naitupa
A. pipi
B. muwa
C. iskrimu
D. firigisi

24. Akisami $\frac{1}{4}$ huitwa
A. robo
B. nusu
C. thumni
D. thuluthi

25. Kinyume cha mzee ni
A. babu
B. nyanya
C. kijana
D. mtoto
26. Tumia kishairia cha mbali sana
Dereva _____ anaendesha.
A. huyo
B. huyu
C. yule
D. hawa
27. Umbo hili huitwa



- A. duara B. kopa
C. mviringo D. duaradufu
28. Ng'ombe _____ wamechinjwa.
A. ipi
B. wapi
C. zipi
D. yupi
29. Ukitaka kupepeta nafaka utatumia
A. buli
B. chano
C. kinu
D. uteo
30. Chagua neno lililoandikwa vizuri
A. radio
B. mschana
C. televishioni
D. ghala

Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 31 – 40.

Hapo kale palikuwa na mzee mmoja na mke. Walikuwa wakiishi karibu sana na bahari. Nyumba yao ilikuwa ni kibanda kibovu tu. Kila siku mzee huyo alikwenda baharini kuvua samaki. Mke alisokota nyuzi nyumbani. Walikuwa wamekwisha kaa hapo kwa muda wa zaidi ya miaka thelathini.

Siku moja mzee huyo alibahatika kuvua samaki mmoja wa dhahabu akafurahi mno. Alipotaka kumkamata, samaki yule alimulika mwangaza mwekundu mbele yake. Samaki yule alibadilika akawa msichana mrembo. Mzee akawa na wasiwasi. Samaki yule alianza kuongea. Alimwambia mzee huyo afanye bidii zaidi na Mungu angambariki. Mzee aliamua kufanya bidii ili afaidike.

- | | |
|---|---|
| <p>31. Mzee aliyesemuliwa alikuwa akiishi na nani?
A. watoto wake B. mke wake
C. wazazi wake D. ndugu yake</p> <p>32. Mzee alifanya kazi gani?
A. kufua nguo
B. kuosha magari
C. kufua samaki
D. kuvua samaki</p> <p>33. Mzee alikuwa amekaa hapo kwa zaidi ya miaka mingapi?
A. mwaka mmoja
B. miaka tisa
C. miaka thelathini
D. maika thamanini</p> <p>34. Samaki aliyevuliwa alikuwa wa aina gani?
A. wa dhahabu
B. wa manjano
C. wa kijani
D. wa hudhurungi</p> <p>35. Mzee alipotaka kumkamata samaki alifanya nini
A. alimuuma
B. alimulika mwangaza
C. alirudi majini
D. alilia sana</p> | <p>36. Samaki alibadilika akawa
A. maji B. chura
C. mpira C. msichana mrembo</p> <p>37. Mzee aliambiwa afanye bidii kwa nini
A. ili Mungu ambariki
B. ili awe samaki
C. ili awe mrembo
D. ili awe tajiri</p> <p>38. Samaki husihi majini. Je, ngombe hushi
A. kimbani B. zizini
C. kiotani D. msituni</p> <p>39. Samaki alitoa mwangaza wa rangi gani?
A. nyeupe B. samawati
C. nyekundu D. nyeusi</p> <p>40. Kulingana na kifungu, ili tufaidike, lazima
A. tuve samaki wa dhahabu
B. tuwe wazee
C. tuwe wenye hasira
D. tuwe na bidii</p> |
|---|---|

Soma ufahamu ifuatayo kisha ujibu maswali 41 – 50.

Ajali nyingi hutokea barabarani. Je, ndiko kusema barabara zetu ni mbovu mno kiasi cha kuwashinda madereva wetu kuendesha magari vizuri? Jibu ni la hasha!

Ajali hizi husababishwa na binadamu wenye magari hayo. Dereva si watu waangalifu wanapoendesha magari ya abiria. Wengine ni walevi wa pombe, miraa, bangi na dawa nyingine za kulevya. Wengine ni dereva wa uongo ambao hawakujifunza udereva katika shule maalum za udereva bali walipata leseni zao kwa njia ya udanganyifu. Wengine wana tamaa ya kupata pesa nyingi.

Ni vyema mtu akiingia kwenye gari na apate dereva ni mlevi ashuke na kupiga ripoti katika kituo cha polisi kilicho karibu. Kwa kufanya hivyo, tutaweza kuwatia adabu madereva ili ajali hizi zipungue. Kweli, watu wengi hupoteza maisha yao katika barabara zetu. Cha kuhuzunisha ni watoto wengi hubaki mayatima wasio na mbele wala nyuma. Tuungane kukomesha ajali katika barabara zetu.

- | | |
|--|---|
| <p>41. Ajali za barabarani zinahusu</p> <p>A. baiskeli</p> <p>B. askari</p> <p>C. wanyama</p> <p>D. magari ya abiria</p> <p>42. Dereva wengine wanatumia dawa za</p> <p>A. kulevya</p> <p>B. kusinzia</p> <p>C. kutibu magogwa</p> <p>D. kulevia</p> <p>43. Dereva huendesha gari. Je, anayeendesha ndege ni</p> <p>A. rubani</p> <p>B. nahodha</p> <p>C. piloti</p> <p>D. rubani</p> <p>44. Ukijifunza kuendesha gari unapewa nini</p> <p>A. leseni</p> <p>B. zawadi</p> <p>C. gari</p> <p>D. pesa</p> <p>45. Ipi si dawa ya kulevya iliyotajwa kwenye kifungu?</p> <p>A. pombe</p> <p>B. bangi</p> <p>A. miraa</p> <p>D. sharubati</p> | <p>46. Watu wanaosafiri hulipa</p> <p>A. karo</p> <p>B. nauli</p> <p>C. kiingilio</p> <p>D. mahari</p> <p>47. Wanaosafiri ndani ya magari huitwa</p> <p>A. utingo</p> <p>B. abiria</p> <p>C. madereva</p> <p>D. askari</p> <p>48. Ajali nyingi za magari hutokea wapi?</p> <p>A. barabarani</p> <p>B. majilisini</p> <p>C. nyumbani</p> <p>D. runingani</p> <p>49. Chombo kipi kati ya hizi husafiria majini</p> <p>A. ndege</p> <p>B. mkokoteni</p> <p>C. pikipiki</p> <p>D. dau</p> <p>50. Kamilisha methali: Tamaa mbele</p> <p>A. Majuto ni mjukuu</p> <p>B. mauti nyuma</p> <p>C. kifo chaja</p> <p>D. ilimwua fisi.</p> |
|--|---|

UJIBU / DAWA